JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

04 **HISABATI**

MUDA: ***Saa 2*** ***Mchana 10 Septemba 2008***

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina **maswali 50.**
2. Jibu maswali yote.
3. Majibu **yote** yaandikwe katika karatasi ya kujibia uliyopewa.
4. Sima za mkononi **hazitaruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika karatasi yako ya kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 7 zenye maandishi

Scanned with CamScanner

NA.	MASWALI	SEHEMU YA KAZI
1.	Tafuta jumla ya namba tasa zote zilizopo kati ya 100 na 110.	
2.	10000 − 11 =	
3.	623 + 5 + 1700 =	
4.	1444 ÷ 38 =	
5.	4563 x 745 x 10 =	
6.	Andika namba inayofuata katika mfululizo huu. $\frac{1}{3}, \frac{2}{9}, \frac{4}{27}, \frac{8}{81}, _____$	
7.	Andika namba mraba ya 13.4.	
8.	Kipi ni kigawo kikubwa cha shirika (KKS) cha 15, 45 na 24?	
9.	$5\frac{1}{2} + 1\frac{1}{6} =$	
10.	4.6 x 30.15 =	
11.	$\frac{21}{25} \div \frac{7}{15} =$	
12.	Andika $3\frac{37}{500}$ kama desimali.	
13.	0.05 ya wanafunzi 55 wa darasa la nne hawakufaulu mtihani wa hisabati. Je ni schemu gani ya wanafunzi wamefaulu mtihani huo?	
14.	$\frac{1}{40}$ inazidi $\frac{1}{50}$ kwa asilimia ngapi?	
15.	Geuza $\frac{2}{3}$ kuwa asilimia.	
16.	Badili 0.25% kuwa schemu rahisi.	

Scanned with CamScanner

NA.	MASWALI	SEHEMU YA KAZI
17.	Mji wa Dar es salaam upo nyuzi 39 mashariki mwa mstari wa meridiani kuu. Andika nyuzi hizo katika mfumo wa namba kamili.	
18.	Iwapo x = +2 na y = -1, tafuta thamani ya $2x - y \div x + y$.	
19.	Andika DCV kuwa namba za kawaida.	
20.	Jumlisha meta $2\frac{1}{2}$, meta 2 na meta 1.25. (Jibu katika m na sm).	
21.	$3\overline{)km16\ m24\ km5}$	
22.	Eropleni iliruka kutoka Dar es Salaam hadi Nairobi kwa mwendokasi wa km 1280 kwa saa. Tafuta umbali kati ya Dar es Salaam na Nairobi ikiwa eropleni ilitumia muda wa saa 1 na dakika 45 kwa safari nzima.	
23.	Iwapo $\frac{1}{5}$ ya akiba yangu ni shilingi 344, tafuta akiba yangu	
24.	Andika jina la pembetatu inayoundwa na majira ya nukta A,B na C. 	

Scanned with CamScanner

NA.	MASWALI	SEHEMU YA KAZI
25.	Wastani wa vimo vya wasichana 4 ni sm 120. Ikiwa vimo vya wasichana 3 ni sm 115, sm 121 na sm 125. Tafuta kimo cha msichana wa nne.	
26.	Grafu ifuatayo inaonyesha kiasi cha mvua iliyonyesha katika kijiji cha Mnadani kwa miezi ya Januari hadi Machi. Je mvua iliyesha kiasi gani (mm) kwa kipindi chote hicho? 	
27.	Wastani wa wanyama ambao hugongwa na magari katika mbuga ya wanyama ya Mikumi kwa miaka 5 ni 27. Tafuta wastani wa wanyama watakaogongwa kwa miaka 11, iwapo wastani wa miaka 6 ni wanyama 25.	
28.	Uwiano wa Y na Z ni sawa na uwiano wa 17 na 19. Tafuta thamani ya Y iwapo Z = 133.	
29.	Uwiano wa mchanga na saruji katika kutengeneza tofali ni mifuko $1\frac{1}{2}$ ya saruji kwa karai 12 za mchanga. Karai ngapi za mchanga zitatumika kwa mifuko 12 ya saruji?	
30.	$2y = \frac{1}{2}y + 6$. Nini thamani ya y?	

Scanned with CamScanner

NA.	MASWALI	SEHEMU YA KAZI
31.	Iwapo a = 2, b = -3. Tafuta thamani ya $\frac{3a-6b}{ab}$	
32.	Rahisisha $3x + 4y - 7x + 5 = 7 - y$.	
33.	Mistari miwili ambayo haikutani inaitwaje?	
34.	Tafuta eneo la pembetatu PQR.  	
35.	Shamba la shule lina urefu wa m 305.25 na upana wa m 205.4. Tafuta eneo la shamba hilo.	
36.	Tafuta eneo la duara lenye nusu kipenyo cha sm 2.8. (Tumia $\pi = \frac{22}{7}$).	
37.	Tafuta eneo la nyuso za mche duara huu uliofungwa pande zote. (Tumia $\pi = \frac{22}{7}$).  	

Scanned with CamScanner

NA.	MASWALI	SEHEMU YA KAZI
38.	Mche mraba una urefu wa sm 7. Tafuta eneo la nyuso zake za nje.	
39.	Tafuta thamani ya pembe X. 	
40.	Pembetatu sawa ina nyuzi 2t kwa kila pembe. Tafuta thamani ya t.	
41.	Mwendesha pikipiki aliendesha umbali wa km 48 kutoka kituo U kuelekea mashariki hadi kituo V, kisha akaelekea kaskazini umbali wa km 20 hadi W. Tafuta umbali kutoka U hadi W.	
42.	Ujazo wa kopo ni lita 3.85. Tafuta nusu kipenyo chake iwapo kimo ni sm 100. (Tumia $\pi = \frac{22}{7}$, sm^3 1000 = lita 1)	
43.	Tafuta ukubwa wa kamusi yenye umbo la mche mstatili wenye urefu wa sm 20, upana wa sm 14 na kimo cha sm 2.	
44.	Tafuta thamani ya Z katika mchoro ufuatao: 	

Scanned with CamScanner

NA.	MASWALI	SEHEMU YA KAZI
45.	Tafuta thamani ya n katika mmbo lifuatalo:  	
46.	Anna alitumia sh. 4600 kutuma simu ya maandishi. Je, alituma maneno mangapi iwapo gharama kwa maneno 20 ya mwanzo ni sh. 30 kwa kila neno na sh. 20 kwa kila neno linaloongezeka?	
47.	Saa ya Janeth ilionyesha saa 2.15 asubuhi. Muda huo ni saa ngapi kwa mfumo wa saa 24?	
48.	Tafuta kianzio ikiwa faida iliyopatikana kwa mwaka mmoja ni sh. 3000 na kiasi cha riba kwa mwaka ni 5%.	
49.	Fadhili alikwenda sokoni na sh. 7000 akanunua vitu vifuatavyo: Nyama kg 2 ½ @ sh. 800, viazi kg 5 @ 600, pilipili hoho ½ kg @ sh. 480 na ndizi 20 @ sh. 50. Je, alibakiwa na kiasi gani baada ya kununua vitu vyote hivyo?	
50.	Basi lilianza safari ya kwenda Iringa saa 1630 na kufika kesho yake saa 0630. Je, basi hilo lilitumia muda gani kwa safari nzima?	

Scanned with CamScanner